

## GHARAMA ZA KUPIMA VIWANJA

Gharama ya Kupima kiwanja ambacho kinaendana na mchoro wa mipango miji.

#	Idadi ya Viwanja	kiasi	Maelezo
1	Kiwanja kimoja	1,700,000/=	Hii pamoja na gharama ya ukaguzi
2	Kiwanja kimoja na Zaidi hadi kumi	1,700,00/= + 700,000/= @ kinachozidi	
3	Kiwanja kimoja hadi mia	1,700,000/= @ +600,000/= kila kinachozidi	
4	Kiwanja kimoja hadi mia tano	1,700,000/= @ +400,000/= kila kinachozidi	
5	Kiwanja kimoja hadi elfu moja	1,700,000/= @ +300,000/= kila kinachozidi	
6	Zaidi ya viwanja elfu moja	Tsh 200,000/= @	

Muda wa kupima na kukamilisha/kuidhinishwa kwa upimaji ni miezi 3

Endapo eneo haliendani na mchoro wa mipango miji mteja atashauriwa kuandaa Marekebisho ( amendment) au mchoro wa eneo lake.

Ambapo gharama za kuandaa Mchoro wa mipangomiji ni kama ifuatavyo;-

#	Eneo	kiasi	
1	Wilaya ya Kigamboni, Temeke, Ubungo na Kinondoni	7,000,000/=	Mchoro 1
2	Wilaya ya Ilala, Bagamoyo na Kibaha	6,000,000/=	
3	Maeneo mengine	5,000,000/=	

Gharama ya kuandaa marekebisho ya mchoro ni Tsh 3,000,000/=

Zoezi la kuandaa mchoro wa mipango miji linahusiana na ratiba za vikao vya halmashauri hivyo mteja atalazimika kusubiri kwa kipindi cha miezi sita.

## HATI MILIKI

Kuandaa hati miliki ya eneo vifuattavyo ni muhimu;-

1. Eneo liwe na mchoro wa mipango mji ili kujua matumizi ya kiwanja
2. Eneo liwe limepimwa ili kujua ukubwa wa kiwanja, mahala lilipo na namba ya usajili wa mchoro
3. Mmiliki awe na mkataba wa manunuzi au umiliki wa eneo.
4. Barua ya serikali za mitaa
5. Cheti cha kuzaliwa
6. Na picha ndogo (passport size) sita  
Zoezi zima la kufuatilia utengenezaji wa hati litachukua miezi mitatu (3)